OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMSHAURI YA MJI KIBAHA

SIMU : 0656 424 336/0789 510 710 (MKUU WA SHULE)
0622 075527 (MAKAMU MKUU WA SHULE)

SHULE YA SEKONDARI MWANALUGALI
S.L. P 30267
KIBAHA – PWANI

……..

KUMB. NA…….
MZAZI /MLEZI WA MWANAFUNZI……
S.L.P …….

YAH : MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANALUGALI KIDATO CHA TANO 2022/2023

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Mwanalugali iliyopo Kibaha mkoa wa Pwani kwa mwaka wa masomo 2022/2023 tahasusi (combination) ya ……. Muhula wa masomo utaanza tarehe …… unatakiwa kuripori shuleni kabla ya saa 11 jioni bila kukosa ukiwa umevaa nguo ya heshima. Mwisho wa kuripoti ni tarehe……

1.1 JINSI YA KUFIKA SHULENI

Shule ya sekondari Mwanalugali ni shule ya Bweni ya wavulana, ipo umbali wa kilometa nne (4km) kutoka maili moja, kushoto mwa barabara kuu itokayo Dar es salaam kuelekea mikoani. Ukipanda basi toka mikoani shuka maili moja stand kuu ya mabasi, usafiri wa kukufikisha shuleni ni pikipiki ambayo inapatikana kwa gharama kati ya tshs. 1500/= na 2000/=

Fomu zote zilizoambatanishwa na maelezo haya zinatakiwa kujazwa kikamilifu. TUNASISITIZA FOMU HII KURUDISHWA BILA KUPUNGUZWA KURASA YOYOTE, ni mategemeo yetu kuwa mwanao atasoma kwa makini na kuzielewa.

1.1 ADA NA MICHANGO YA SHULE.

NA	MICHANGO	KIASI
1	Ada ya shule	70,000.00 kwa mwaka 35,000.00 kwa muhula
2	Taaluma	20,000.00 kwa mwaka
3	Tahadhari	5,000.00 (haitarejeshwa)
4	Huduma ya kwanza	10,000.00 kwa mwaka
5	Walinzi/ wapishi	30,000.00 kwa mwaka
6	Kitambulisho	6,000.00 mara moja
7	Mitihani ya kujipima na mock	20,000 kwa mwaka
8	Ukarabati	15,000 hulipwa mara moja
	JUMLA	**176,000/=**

Fedha hizi zilipwe kwenye akaunti ya shule NMB A/C Na. 21201200150 jina la akaunti ni MWANALUGALI SECONDARY SCHOOL RECURRENT. Mwanafunzi aje na pay in slip shuleni siku anayoripoti ikionyesha jina kamili la mwanafunzi na tahasusi yake. Hakikisha unabaki na nakala moja ya bank pay in slip.

NB. MALIPO YOTE YA SHULE YALIPWE BANK. HATUPOKEI PESA TASLIMU ZA ADA NA MICHANGO YA SHULE ILIYOORODHESHWA HAPO JUU KATIKA JEDWALI.

2.0 SARE YA SHULE

- Suruali mbili rangi ya **Light Grey (**Esteem No 1**)** kitambaa cha suti zilizoshonwa na selebration (marinda mawili) yenye upana inch 14 na turn up, ziwe zimeshonwa kwa heshima na zisiwe za kubana (MODAL) kwa ajili ya darasani, na suruali moja ya **Dark** blue kwa ajili ya kushindia na kazi za nje, haya ndio yatakuwa mavazi yake kipindi chote atakachokuwa shuleni, hataruhusiwa kuvaa nguo za nyumbani (unaweza kuja kushona shuleni).

- Shati mbili nyeupe mikono mifupi
- Tai rangi ya **grey** (inapatikana shuleni)
- Soksi nyeusi jozi 2 zisiwe na marembo
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba na visiwe buti
- T- shirt mbili rangi ya **brown** (inapatikana shuleni)
- Sweta moja rangi ya **grey** (inapatikana shuleni)

2.2 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

- Bunda (ream la karatasi **A4**) mbili kwa mwaka
- Madaftari makubwa counter books sita (6) yanapatikana duka la shule
- Mathemarical set,scientific calculator kwa watakao soma geography na mchepuo wa sayansi.
- Oxford advanced learner's dictionary moja (1) na kamusi ya Kiswahili sanifu moja (1) kwa watakaosoma masomo ya lugha
- Kalamu za blue na nyeusi za kutosha na penseli
- Vifaa vya michezo raba, na (jezi za **light blue** zinapatikana shuleni**)**
- Shuka mbili (2) za **light blue** na chandarua cheupe
- Mto na foronya za **light blue**
- Track suit moja ya rangi ya **grey** kwa ajili ya masomo ya jioni (evening preparation inapatikana shuleni.
- Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na sabuni za kutosha za mche na za unga
- Vyombo vya chakula, ssahani, bakuli,kikombe,kijiko vyote vya **aluminium** (chuma)
- Godoro la futi mbili na nusu kwa sita ($2^{1/2}$ x 6) (yanapatikana shuleni).
- Sanduku la bati na kufuli za kufungia sanduku lake
- Ndoo ndogo mbili zenye mfuniko rangi ya blue au nyekundu.

- Vifaa vya usafi : kila mwanafunzi alete vifaa vya usafi kama ilivyoainishwa hapa chini kwa kila tahasusi;-

1. PCM : jembe na kwanja
2. HGL : Soft broom,reki 1, hard broom,
3. Kila mwanafunzi aje na vitabu muhimu kulingana na masomo anayosoma.
4. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu ya mkononi,heater,jagi la kuchemshia maji hapa shuleni/bwenini
5. Kila mwanafunzi aje na cheti cha kuzaliwa
6. Kila mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya kwa ajili ya matibabu

NB. 1. VIFAA VYOTE VITAKAGULIWA WAKATI WA KUMPOKEA MWANAFUNZI, TUNASISISITA KUZINGATIA MAELEKEZO HAYA.

NAKUTAKIA KILA LA KHERI NA MAANDALIZI MEMA.

JOSEPH M. MKUMBO
MKUU WA SHULE.

SHERIA ZA SHULE

Katika jamii yoyote ile ni lazima kuwepo na SHERIA, KANUNI NA TARATIBU zitakazo wezesha jamii hito kuishi kufuata maadili mema na mazuri ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

1. MAHUDHURIO

I. Wanafunzi wote wawapo shuleni ni lazima waisome, waielewe na waifuate kwa makini ratiba ya shule kila siku.
II. Kwa kuwa lengo ni kupata elimu, wanafunzi wote ni lazima wahudhurie na kuwahi vipindi vya darasani, vipindi vya elimu ya kujitegemea na vipindi vya michezo na shughuli zingine zozote za shule kama zitakavyopangwa katika ratiba, isipokuwa ruhusa ya kutokuwepo itatolewa.
III. Iwapo mwanafunzi atakosa shule kwa sababu yoyote bila ruhusa ni lazima siku inayofuata aje na taarifa ya maandishi kutoka kwa mzazi/mlezi au daktari kuelezea sababu za msingi zilizomfanya asihudhurie shule siku hiyo/hizo.
IV. Endapo mwanafunzi hatahudhuria shuleni kwa siku 30 mfululizo bila taarifa atasimamishwa masomo, na kufukuzwa shule kwa kutokuhudhuria siku 90.
V. Pia mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule kwa kukimbia/kutohudhuria na kutofanya mitihani
VI. Pia mwanafunzi hatoruhusiwa kutoka nje ya mazingira ya shule bila ya kibali maalumu kitakachotolewa na mwalimu wa zamu au mlezi.
VII. Wanafunzi wote wanatakiwa kufuata ratiba ya shule ya siku kwa usahihi kuanzia 1 :20 asubuhi mpaka saa 9 :30 alasiri au kama itakavyoeleza vinginevyo.
VIII. Wanafunzi wote wanatakiwa kushiriki kikamilifu shughuli zote baada ya ratiba ya darasani kama elimu ya kujitegemea, clubs, mdahalo,michezo,na usafi wa mazingira.

2. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

Kuvunja miiko ifuatayo inaweza kusababisha mwanafunzi kupata adhabu kali, kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule kabisa.

I. Utoro
II. Uzururaji
III. Uasherati
IV. Wizi na uwongo
V. Kuvuta bangi, kutumia dawa ya kulevya au ulevi wa aina yoyote ile
VI. Kuchezea ,kuharibu au kudharau alama za Taifa kama bendera na wimbo wa Taifa
VII. Kupigana au kutukana
VIII. Kutoa lugha ya matusi kwa yotote yule
IX. Kugomea masomo,adhabu au maagizo yaliyotolewa na mwalimu
X. Fujo, uchochezi na kupelekea uvunjivu wa amani

XI. Kutofanya mitihani au mazoezi kwa makusudi bila taarifa maalum
XII. Kuficha maovu,wahalifu na uhalifu
XIII. Makosa ya jinai
XIV. Kushiriki kutoa mimba
XV. Kusababisha mimba ndani na nje ya shule
XVI. Kuoa au kuolewa
XVII. Kutumia vibaya mali ya umma na hivyo kusababisha uharibifu na hasara
XVIII. Kukutwa na simu maeneo ya shule.
XIX. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ya kibali cha mwalimu anayehusika na malezi ya mwanafunzi au mwalimu wa zamu.

NB : UPOTEVU AMA UHARIBIFU WA VIFAA VYA SHULE VITALIPWA NA MHUSIKA KWA GHARAMA HALISI YA VIFAA HIVYO AU KIFAA CHENYEWE.

3. HESHIMA

I. Wanafunzi wote wanatakiwa kutii kengele
II. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa kwa unadhifu na usahihi na kuchomekea wakati wowote wanapokuwa katika sare ya shule. ATAKAYEVAA MODAL ITAKATWA NA KUTEKETEZWA ILI KULINDA HESHIMA NA MAADILI YA TAIFA. Tunasisistiza heshima katika mavazi.
III. Wanafunzi wote wanatakiwa kusimama paredi kwa unadhifu na ukakamavu
IV. Wanafunzi wasimame kusalimia walimu au mgeni aingiapo darasani
V. Wanafunzi wasitoke darasani bila ruhusa na kwa makundi makundi
VI. Wanafunzi wasipige kelele darasani
VII. Wanafunzi waheshimiane wao kwa wao na waheshimu viongozi
VIII. Hairuhusiwi kuzomea darasani au nje ya darasa
IX. Wanafunzi wawaheshimu wafanyakazi wengine waliopo shuleni pamoja na maeneo jirani yanayozunguka shule.
X. Wanafunzi wawe katika mfano bora katika fani zote, heshima, kazi na usafi hata wanapokuwa nje ya mazingira ya shule.
XI. Wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi na nadhifu
XII. Wanafunzi hawaruhusiwi kufuga ndevu.

4. MIPAKA YA SHULE

I. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali. Wanafunzi watakaoishi Hostel/Bweni hawataruhusiwa kutoka nje ya maeneo ya shule mara watakapopokelewa shuleni mpaka shule itakapofungwa au kibali maalum kama kwenda kanisani, msikitini na hospitali kwa muda maalum , pia wanafunzi hawaruhusiwi kufika sehemu zifuatazo isipokuwa kwa ruhusa maalum.

a. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
b. Ofisi zote za shule bila sababu maalum
c. Maabara bila sababu maalum

d. Jikoni

II. Wanafunzi hawaruhusiwi kufika sehemu zifuatazo.
   a. Vilabu vyote vya pombe
   b. Majumba ya kufikia wageni
   c. Majumba ya starehe
   d. Makazi ya watu (majirani) bila ruhusa au sababu maalum

5. CHAKULA

Chakula cha wanafunzi kitapatikana shuleni, hakutakuwa na chakula maalum wanafunzi wote watakula chakula kilicho idhinishwa na shule.

6. MABADILIKO YA MAJINA NA ANUANI

I. Endapo jina na anuani ya mzazi/mlezi vitabadilishwa kwa sababu yoyote taarifa itolewe shuleni ili rekodi za shule ziwe sahihi wakati wowte na hasa wakati wa kupokea taarifa mbalimbali kwa mzazi/mlezi kuhusu maendeleo ya mwanafunzi.

II. Majina ya wanafunzi yaliyopokelewa shuleni ndiyo yatakayotumika bila kubadilishwa

7. TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi kama lilivyotumika katika mtihani wakidato cha nne

   ……
   ……

2. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi.

   Tarehe…… Mwezi……
   Mwaka……..

3. Mahali alipozaliwa mwanafunzi

   - Kijiji…….
   - Wilaya……..
   - Mkoa…….
   - Kabila la mwanafunzi……..
   - Jinsia ya mwanafunzi……
   - Dini……
   - Jina la mzazi/mlezi……..
   - Namba ya simu…….
   - Majina ya ndugu wengine wawili

     (1)Jina…… uhusiano

     …….. namba ya simu

     (2)Jina…… Uhusiano…….Namba ya simu……..
   - Je ana ugonjwa sugu/ulemavu ? kama ndiyo taja……
   - Njoo na uthibitisho wa daktari toka hospitali ya serikali
   - Sahihi ya mzazi/mlezi……..
   - Tarehe…….

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING
KIBAHA TOWN COUNCIL
MWANALUGALI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 3026 KIBAHA

STUDENTS MEDICAL EXAMINATION FORM
TO THE MEDICAL OFFICER IN CHARGE
Please, examine the under named student and note any medical complication towards him.
Students Name……
Age…….. Class……

JOSEPH M. MKUMBO
THE HEADMASTER
MWANALUGALI SEC,SCHOOL.

1. Blood (Any infection noted)……..
2. Blood Group……
3. Stool…….
4. Urine Analysis……..
5. Eyes (Any eye defect)……..
6. Chest……..
7. Abdomen…….
8. Heart Diseases……

Any chronic complaints needs attention of school authority……

Name of the medical officer…….

Signature……

Designation…….

Station…….

Date……

Official Stamp……..

OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

YAH : Hati ya kukubali masharti kuhusu mtoto wangu kusoma shule ya sekondari Mwanalugali.

Mimi……..

Mzazi/Mlezi wa ……..

Aliye kuwa akisoma shule ya

……

Katika wilaya ya

……..

Mkoa wa ……..

Ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari mwanalugali iliyoko katika mji wa kibaha kwa kuzingatia masharti yafuatayo

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria kama kawaida na atafanya shughuli nyingine zote za shuleni kwa kipindi chote cha miaka miwili cha kidato cha tano na cha sita.
2. Kwamba kwa muda wote huo wa miaka miwili sitamsumbua mkuu wa shule, afisa elimu sekondari wilaya,na mkoa kuomba uhamisho

   Sahihi ya mzazi/mlezi……
   Tarehe……..
   Ahadi ya mwanafunzi
   Mimi……..
   Nimekubali nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari mwanalugali, nina ahidi kuwa mtiifu na kufuata kikamilifu sheria , kanuni na taratibu halali zilizopo, pia ninaahidi kufanya bidii na kushirikiana na uongozi wa shule na wanafunzi katika kuendeleza taaluma na shughuli zingine nitakazo pangiwa.
   Sahihi…….
   Jina…….
   Tarehe……..

Nakala.

1. Mkurugenzi wa halmashauri
   S.l.p 30112
   Kibaha

2. Afisa elimu mkoa
   S.l.p 30080
   Kibaha

3. Mkurugenzi
   Elimu sekondari
   Tamisemi

4. Mkurugenzi
   Elimu ya sekondari
   Wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi
   S.l.p 9121